



TANGAZO KWA VYOMBO VYA HABARI

Benki Kuu yatoa sarafu ya kumbukumbu ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar

Benki Kuu ya Tanzania imetoa sarafu maalum ya kumbukumbu ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye thamani ya shilingi elfu hamsini (Sh. 50,000), alitangaza Gavana Profesa Benno Ndulu.

Hata hivyo, alisema sarafu hiyo iliyotengenezwa kwa madini ya fedha kwa asilimia 92.50, imetolewa kwa ajili ya kumbukumbu tu na haitaingizwa katika mzunguko wala kutumika kwa kulipia malipo ya aina yoyote.

Profesa Ndulu alisema sarafu hiyo imetolewa kwa idadi ya vipande elfu tatu (3,000) kwa ajili ya tukio hilo muhimu la kumbukumbu ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aliwahimiza wananchi kuinunua kwa ajili ya kumbukumbu hiyo.

Kwa mujibu wa Gavana, kutolewa kwa sarafu hii kunakwenda sambamba na utaratibu wa Benki Kuu kutoa sarafu maalum za aina hii kama sehemu ya maadhimisho ya kumbukumbu ya matukio mbalimbali muhimu ya kitaifa na kimataifa. “Kwa kawaida, baada ya muda, thamani ya sarafu kama hizi huongezeka na kuwa na faida zaidi kwa wanaozimiliki,” alisema Profesa Ndulu.

Gavana Ndulu alifafanua kwamba sarafu hizi zitapatikana kuanzia tarehe 5 Januari 2014 kwa bei ya shilingi elfu hamsini (Sh. 50,000) katika matawi ya benki za biashara zitakazokuwa zimeweza

kupata sarafu hizi kutoka Makao Makuu ya Benki Kuu jijini Dar es Salaam na matawi ya Benki Kuu yaliyoko Zanzibar, Arusha, Mbeya na Mwanza.

“Benki za biashara zinaweza pia zikasambaza sarafu hizi kupitia matawi yake,” alisema Gavana na kuongeza kwamba taarifa za usambazaji zitatolewa na benki hizo.

Upande wa mbele wa sarafu hiyo unaonyesha sura ya hayati Sheikh Abeid Amani Karume, na maandishi yanayosomeka ‘Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi’. Upande mwingine wa sarafu unaonyesha nembo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, maandishi yanayosomeka “Miaka Hamsini ya Mapinduzi”, thamani ya sarafu na miaka 1964-2014.

Imetolewa na Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki

Januari 1, 2014